# Ukweli wa Injili

Mafundisho ya Biblia na Himizo kwa Kazi ya Kimisheni Ulimwenguni Kote

## WITO WA KUFANYIKA KWA HAKI NA JAWABU LA REHEMA

Kuna mwanamke mmoja aliyeletwa kwa Yesu na Mafarisayo. Alikuwa ameshikwa katika tendo la uzinzi. Ushahidi uliokuwapo ulikuwa dhabiti kabisa na usio na tashwishi. Ndipo mwanamke huyo akasubiri kulaaniwa na kuhukumiwa kwake, na kulingana na sheria hukumu yake ilikuwa ya hakika. Lakini Yesu Mwana wa Mungu akampa ujumbe tofauti, "Wala mimi sikuhukumu. Enenda zako; wala usitende dhambi tena" (Yohana 8:11).

Hapo mwaka 760 Kabla ya Kristo (KK) kulikuwa mji uliokuwa na maovu mengi ulioitwa Ninawi. Katika mji huo mkuu wa watu wa Ashuru kulikosekana utaua kabisa kabisa. Badala yake mji huo ulijaa ibada za sanamu, mambo mapotovu ya kingono, matendo ya kimwili, uongo, unyakuzi wa mali, matumizi ya mabavu, na uchawi. Ndiposa Mungu akamtuma nabii Yona kutangaza hukumu yake ambayo ilikuwa imekaribia, kwamba Mungu angeuangamiza mji huo. Lakini mfalme na watu wake wakatubu na kumwomba Mungu kuwarehemu. Naye Mungu akaacha hukumu yake, na hakuangamiza mji huo (Yona 3).

Yesu anahadithia hadithi ya kijana mmoja katika Luka 15 ambaye alimwasi baba yake. Kijana huyu alitorokea mambo mazuri ya hapo nyumbani, na akufuja mali yake kwa kuishi maisha ya uovu. Lakini akajipata pabaya huku akiwa amejaa dhambi maishani mwake. Aliporudiwa na fahamu zake, akaondoka kuelekea nyumbani, huku akiwa na mpango wa kumwomba baba yake ampokee kama mmoja wa watumishi wake. Lakini baba alikuwa akitazamia siku ambayo kijana huyo angerudi nyumbani na akamkaribisha kwa mikono miwili. Kijana huyu mpotevu akasamehewa na kurejeshewa mahali pake humo nyumbani kama mwana.

Muda baada ya mwingine wana wa Israeli walikataa kumtii Mungu na kufuata njia zao za uovu. Lakini mara baada ya nyingine Mungu aliwasamehe na kuwarudishia hadhi yao kama taifa. "Ila kwa rehema zako nyingi hukuwakomesha kabisa, wala kuwaacha; kwa maana wewe u Mungu mwenye neema, mwenye rehema" (Nehemia 9:31).

Na wakati ule Kristo alikuwa akifanyiwa kesi na mwishowe kusulubiwa Mtume Petro alimfuata kutoka mbali. Alipoulizwa kama yeye ni mfuasi wa Yesu, Petro alikana kumjua Yesu kabisa kabisa. Akamkana mara tatu. Mara ya tatu Yesu akageuka na kumtazama Petro, ambaye sasa alitoka humo na kulia kwa uchungu. Lakini wakati Yesu alifufuka kutoka kwa wafu, alituma ujumbe wa moja kwa moja kwa Petro kumjulisha kuhusu kufufuka kwake. Yesu akamsamehe Petro, na baada ya siku hamsini Petro alionekana akihubiri Injili hapo katika siku ya Pentekote.

Mfalme Daudi alitenda dhambi na Bathsheba na pia akapanga kwamba mume wake auawe vitani. Wakati dhambi yake ilidhihirishwa, Daudi aliomba na kusema: "Ee Mungu, unirehemu, sawasawa na fadhili zako" (Zaburi 51:1). Mungu akamsamehe Daudi.

Naye Sauli, ambaye baadaye alijulikana kama Paulo, alikuwa amewaua na kuwafunga korokoroni Wakristo wengi. Alikuwa mtu aliyekufuru na mtesi wa Wakristo, lakini ingawa hivyo, aliweza kupata rehema alipomtambua Yesu kama Masihi.

Rehema za Mungu kwa watu wa mataifa zilidhihirika mara baada ya nyingine. Mungu alichelewesha kurudi kwa uzao wa Abrahamu kurithi urithi wao katika nchi ya Kanaani

*(Endelea katika Ukurasa 2)*



"Ila kwa rehema zako nyingi hukuwakomesha kabisa, wala kuwaacha; kwa maana wewe u Mungu mwenye neema, mwenye rehema" (Nehemia 9:31).


| Tahariri | Mafundisho ya Biblia: Rehema | Mwingi wa Rehema | Maswali na Majibu | Je, Wajua? Neno Linalofaa kwa Msimu Huu |
|---|---|---|---|---|
| 3 | 4 | 5-6 | 7 | 8 |

# MAMBO AMBAYO BIBLIA INAFUNDISHA KUHUSU...

**Neno la Mungu**
2 Tim. 3:6, 2 Pet. 1:20-21, Mt. 24:35

**Uhusiano wa Upendo**
Mt. 22:37-40, Yn. 14:21-23, 1 Yoh. 4:7-21

**Toba**
Mdo. 3:19, 17:30, 2 Kor. 7:10

**Uzao Mpya**
Yn. 3:3-7, 2 Kor. 5:17, Rum. 6:1-4, Efe. 2:1, 5-6

**Uhuru Kutokana na Dhambi**
1 Yoh. 5:18, Mt. 1:21, Yn. 8:11

**Ujazo wa Roho Mtakatifu**
Mdo. 19:2, 15:8-9, 1:8

**Utakatifu**
Lk. 1:73-75, Ebr. 12:14, 1 Pet. 1:15-16, Tit. 2:11-12, Rum. 6:22

**Ufalme wa Mungu**
Lk. 17:20-21, Rum. 14:17, Yn. 18:36

**Kanisa**
Mdo. 2:47, Efe. 4:4-6, 1 Kor. 12:12-13, Kol. 1:18

**Umoja**
Yn. 17:20-23, Gal. 3:28, Ufu. 18:2-4

**Kanuni za Kanisa**
Mt. 28:19-20, 26:26-30, I Kor. 11:23-27, Yn. 13:14-17

**Uponyaji wa Kiungu**
Lk. 4:18, Isa. 53:4-5, Yak. 5:13-16

**Utakatifu wa Ndoa**
Mt. 19:5-6, Lk. 16:18, Rum. 7:2-3, I Kor. 7:10-11

**Urembo wa Nje**
I Tim. 2:9-10, I Kor. 11:14-15, Kum. 22:5

**Mwisho wa Nyakati**
2 Pet. 3:7-12, Yn 5:28-29, 2 Kor. 5:10, Mt. 25:31-46

**Kupenda Amani**
Lk. 6:27-29, 18:20

**Ibada**
Yn. 4:23-24, Efe. 5:19, 2 Kor. 3:17

**Wajibu Mkuu**
Mk. 16:15

*(Inaendelea kutoka Ukurasa 1)*

kwa sababu uovu wa Waamori haukuwa umekamilika (Mwanzo 15:16). Waamori walikuwa watu waovu kabisa lakini Mungu alichelewesha hukumu yake na kuwapa muda zaidi, na pia kuwanyooshea mkono wa rehema.

Hadithi hizi fupi za Biblia zina kitu ambacho kinafanana na ambacho kinazifunganisha. Hadithi hizi zinadhihirisha rehema za kweli na halisi za Mungu. Kulikuwa na wito mkubwa kwa hukumu kufanyika, na adhabu ambayo ingetolewa ingekuwa ya haki, lakini badala yake rehema ndizo zilitolewa. Mungu hakuwapa, na hata leo Yeye hawapi watu kile ambacho wanastahili maishani haya. Ila Yeye ni mvumilizu na ni mwenye kupenda kunyoosha mkono wa rehema. Na mkono huo wake wa rehema ungali umenyooshwa kwa watu wa kizazi hiki. Waasi, wenye dhambi, waovu, na wasiostahili kamwe hawaishi bila kuwa na tumaini, kwa maana Mungu ni Mungu wa rehema na msamaha.



Rehema zake Mungu zinahitaji kuenea na kufanya kazi katika maisha ya watu wote. Hapo mwaka wa 2007 kuna mtu mmoja alikuwa akisafiri kwa gari na familia yake. Ndipo hapo wakagongwa na dereva aliyekuwa mlevi. Mume huyo na baba wa watoto wawili akatazama nyuma na kuona kwamba watoto wake wawili walikuwa wameaga dunia. Naye mke wake ambaye alikuwa amekaa kando yake garini huku akiwa na uja uzito wa mtoto wao ambaye bado kazaliwa, alikuwa pia keshakufa. Na alipotazama kupitia kwa kioo cha gari yake ambacho kilikuwa kishavunjika, na kutazama gari lililokuwa likiendeshwa na dereva mlevi, alihisi wito wa Mungu wa kumsamehe mtu huyo na kutokuwa na kinyongo naye. Ndipo hapo akamnyoshea mkono wa rehema na msamahe kijana huyo, ambaye alikuwa akiendesha gari huku akiwa mlevi, na aliyesababisha kifo cha familia yake.

Miaka mingi iliyopita mhudumu wa Injili wa Kanisa la Mungu aliuawa kwa njia ya mabavu. Muuaji huyo alikamatwa na kuwekwa korokoroni. Lakini familia ya mhudumu huyo ikatoa ushahidi kwamba ilikuwa imemsamehe yule bwana ambaye alimuua baba yao.

Je, ni mambo gani mabaya tumefanya na ambayo yalistahili kupata adhabu? Je, umetenda dhambi dhidi ya Mungu kwa njia gani. Je, ni majeraha gani ambayo watu wale wengine wako nayo kutokana na matendo yako? Kama vile ambavyo Mungu ametusamehe kwa neema zake, sisi nasi tunastahili kuwasamehe walio karibu nasi. Wakati watu wametutendea mambo mabaya na kuleta uchungu maishani mwetu, huenda wao wasistahili rehema na msamaha wetu, lakini hata nasi hatukustahili hayo kutoka kwake Mungu. Wakati watu wale wengine wanapofanya wito wa kufanyika kwa haki, hebu wito wetu uwe ni wa rehema. Hebu basi tuwe watu wastahimilivu na wa kuwanyooshea wale wengine rehema badala ya hukumu. Hebu tuwe kioo cha uso wa Mungu kwa njia ya kuwasambazia wengine upendo wake, kwa njia ya matendo halisi ya kuwarehemu watu. Watu wale wengine wanapotaka mtu fulani ahukumiwe, hebu wewe fanya wito wa kutolewa kwa rehema. Wakati watu wengine wanasema hukumu itolewe, hebu wito wako uwe ni wa kuleta uponyaji.

Baba yetu wa Mbinguni ameturehemu, nasi tunastahili kufanya hivyo kwa watu wale wengine kwa njia ya neema zake. ■

Gazeti la *Ukweli wa Injili* ni jalida ambalo linatolewa kila robo ya mwaka kwa manufaa ya Kanisa la Mungu kwa ajili ya mafundisho na kwa ajili ya kuwahimiza Wakristo ili washike kweli za Biblia. Tutembelee katika tovuti yetu ya *www.thegospeltruth.org* na ujiandikishe ili uwe ukitumiwa notisi kwa njia ya barua pepe kila wakati jalida hili likiwa tayari ili uweze kupata toleo la kila kipindi. Gazeti hili la *Ukweli wa Injili* linachapishwa katika nchi nyingi ili lisambazwe katika nchi hizo. Kazi hii inawezekana kupitia kwa matoleo yanayotolewa kwa hiari. Pia wewe ukitaka unaweza kutumiwa risiti ya vile tumelipa ushuru kutokana na zawadi yako.

—Mhariri, Michael Smith

Gospel Truth, P.O. Box 2042, Nixa, MO 65714 USA
editor@the gospeltruth.org

# Tahariri



*Rehema na kweli zisifarakane nawe; zifunge shingoni mwako; ziandike juu ya kibao cha moyo wako.* —Mithali 3:3

Ewe msomaji wangu ninakuomba kama alivyoomba Solomoni, "Rehema na kweli zisifarakane nawe." Ni dhahiri kwamba ulimwengu wetu uko gizani kubwa ya dhambi, na kuna haja ya mwangaza wa ukweli kung'ara kabisa. Hebu basi wewe shikamana na ukweli na uishi kwa ukweli, lakini sio kwa ukweli peke yake. Shikamana pia na rehema zake. Rehema za Mungu ndizo zilituokoa, na rehema zile tunawaonyesha watu wale wengine zitawaongoza ili wajue tumaini ambalo linapatikana katika Yesu Kristo.

Somo la robo hii ya mwaka ni "Rehema." Kwa kweli niliathirika kwa kiwango kikubwa nilipokuwa nafanya utafiti katika Maandiko na kutafakari kuhusu somo hili. Kuna maandiko mengi ambayo yanafundisha na kudhihirisha umuhimu wa rehema, na kwamba ni kitu cha lazima. Ni muhimu kuzingatia kwamba, kuna mengi zaidi ambayo yamesemwa kuhusu umuhimu wa rehema kuliko idadi ya yaliyosemwa kuhusiana na mafundisho ambayo baadhi yetu tumeshika sana. Kama tulivyosema hapo awali, hebu tushikamane na ukweli, lakini pia tusiachane na rehema.

*Tutembelee www.thegospeltruth.org ili kujiandikisha na kupata jarida za mbele.*

Bila rehema zake Mungu hakuna hata mmoja wetu ambaye angeliokoka. Sisi hatukustahili upendo wake Mungu, lakini Yeye alitupenda. Hata baada ya kuanza safari yetu na Bwana, rehema zake ndizo hutudumisha, kwa maana sisi sote hufanya makosa na kupotoka mara moja au nyingine. Kuishi maisha ya ushindi ndicho kiwango ambacho tumewekewa na Biblia, na maandishi haya hayafanyi juhudi zozote za kutuhimiza tuingiliane na mambo ya kidunia, au kuishi maisha yasiyofaa. LAKINI, ni wangapi wetu hatujalazimika kurudi kwake Bwana kumwomba msamaha? Mimi niliokolewa kwa rehema zake, na nimefika mahali nimefika sasa kwa neema ya rehema zake, ambazo ameninyooshea kutokana na makosa yangu na kutokuwa mkamilifu. Kwa sababu kumuishia Mungu ni kuishi maisha ya mtu kuendelea kukua kila siku, daima kutakuwa mahali ambapo tutahitaji rehema zake.

Ninapotafakari kuhusu rehema ambazo Mungu amewaonyesha watu kwa miaka nenda rudi, mimi nashangaa na kupata changamoto maishani mwangu. Kwa kweli ninakumbuka nikirudi kutoka safari ya kimisheni na kuwa na mawazo kwamba, "Nimefika mwisho. Mimi sitorudi kwa watu hao wa kimwili." Lakini Mungu akanena nami na kunikumbusha kuhusu mfano wa mtini ambao haukuzaa matunda, na ambao unatajwa katika Luka 13. Mungu hakuwa amemaliza kazi yake, na ndiposa nikapata kuona kina cha rehema zake. Kusema kweli rehema zangu zilienezwa kwa njia ya neema zake.

Katika ulimwengu wa kidini utapatana na mashirika mengi ya watu wenye mawazo kwamba wao wana uhuru, na ambao wanafundisha kuhusu upendo na rehema, lakini ndani ya mahubiri hayo kuna ukweli mdogo sana. Hayo pia ni makosa. Lakini pia ni makosa kwetu kupeperusha bendera ya ukweli na utakatifu, huku tukiwa hatuna roho ya rehema. Wakati kijiji cha Wanasamaria kilikataa kutembelewa na Kristo, wanafunzi walitaka kuita moto ili uwachome. Lakini Yesu akawaambia, "Hamjui ni roho ya namna gani mliyo nayo" (Luka 9:55). Mimi nimetazama na kuona kwamba kuna roho ya kutoa hukumu ambayo iko na watu wengi wa "utakatifu." Wakati tuko tayari kuwakosoa wale wengine kwa njia ya kuwa na misimamo mikali, basi hapo kunakosekana upendo na rehema. Jambo la kushangaza ni kwamba, inaweza kuwa vigumu kuwarehemu watu ambao wako na haraka ya kuwahukumu wale wengine.

Ni jambo la baraka maishani mwetu na kwa maisha ya watu wale wengine ikiwa tutakuwa watu wa rehema. Rehema ni zaidi ya mafundisho ya Biblia; ila ni matendo halisi ya kuwapenda, kuwasamehe, kuwavumilia, na kutafuta mapatano na watu wale wengine n.k. Hebu basi Mungu atusaide sote ili tupate kuwa watu wenye rehema zaidi na wenye kupunguza hukumu juu ya wenzetu, lakini pia bila kuupotosha ukweli.

Michael W. Smith

Aprili, 2024


**PAKUA**

PROGRAMU

Hii ni rasilmali bora ya kujifunza Biblia na kumsaidia Mkristo kuelewa mafundisho ya Biblia.

GET IT ON Google Play






# Mwongozo wa Kujifunza Biblia

## Somo: Rehema

**Masomo ya Maandiko:** *Lakini wewe, Bwana, U Mungu wa rehema na neema, mvumilivu, mwingi wa fadhili na kweli.* —Zaburi 86:15

**Maana:** Tovuti ya vocabulary.com inasema kwamba rehema ni mwelekeo wa mtu kuwa mwenye huruma, kuwa tayari kutoa msamaha; ni hisia ambazo huwa ni chimbuko la matendo ya huruma; ni hali ya huruma na kuonyeshwa wema kutoka kwa mtu au idara ambayo imesimamia maswala ya kufanyika kwa haki.

**Muhstasari:** Mungu ni mwingi wa rehema na huruma, na Yeye hucheleweshea hukumu yake, na anawapa watu nafasi ya kupata msamaha na kurudishwa kwake. Watoto wa Mungu nao wanahitaji kuwashughulikia wenzao na kushirikiana nao kutokana na misingi ya roho yenye rehema.

### I. Sifa Ya Mungu

A. 2 Wakorintho 1:3-4 Mungu, Baba wa rehema.
B. Danieli 9:9 Rehema na msamaha ni kwa Mungu.
C. Kumbukumbu 4:29-31 Mungu ni Mungu wa rehema.
D. Mika 7:18 Mungu hufurahia rehema.
E. Mathayo 9:36 Yesu ni mwenye huruma.

### II. Rehema Zake Mungu ni Nyingi na za Kudumu

A. Zaburi 103:8 Mungu amejaa huruma.
B. Zaburi 51:1-2 Wingi wa rehema.
C. 1 Mambo ya Nyakati 16:34 Fadhili zake ni za milele.
D. 2 Petro 3:9 Hapendi mtu yeyote apotee.

### III. Wote Wamefanya Dhambi na Wanastahili Hukumu

A. Warumi 3:23 Wote wametenda dhambi.
B. Warumi 6:23 Mshahara wa dhambi ni mauti.

### IV. Hatustahili Rehema Zake Ila Zinatokana na Mapenzi Yake Mungu

A. Waefeso 2:4-6 Rehema sio kwa ajili ya kustahili kwetu.
B. Warumi 9:15-16 Rehema zinatokana na mapenzi yake Mungu.

### V. Wokovu na Uzima wa Milele Unatokana na Rehema

A. Luka 1:78-79 Nuru ya injili ilikuja kwa njia ya rehema zake Mungu.
B. Tito 3:4-7 Wokovu haupatikani kwa matendo bali ni kwa rehema.
C. Isaya 55:7 Mungu huwasamehe watu wabaya.
D. 1 Petro 1:3-4 Rehema za Mungu hutupatia tumaini la Mbinguni.

### VI. Rehema Ndizo Huwadumisha Watu wa Mungu

A. Zaburi 94:18 Fadhili za Mungu huwategemeza wanaoteleza.
B. Maombolezo 3:21-23 Ni kutokana na huruma za Bwana hatuangamii.

### VII. Kuhani Mkuu Mwenye Rehema

A. Waebrania 2:16-18 Yesu ni kuhani mkuu mwenye rehema.
B. Waebrania 4:15-16 Rehema zapatikana kutoka kiti cha rehema.

### VIII. Mwisho wa Rehema za Mungu

A. Yohana 12:48 Wakataao wapata hukumu.
B. Mathayo 25:45-46 Adhabu ya milele kwa wale wasio waaminifu.
C. Waebrania 10:28-29 Kufa pasipo huruma.

### IX. Tumeitwa Ili Tuishi Maisha ya Rehema

A. Luka 6:36 Kuweni na huruma kama Mungu alivyo wa huruma.
B. Mika 6:8 Kupenda rehema.
C. Zekaria 7:9 Kuonyesha rehema na huruma.

### X. Rehema Ni Bora Kuliko Sadaka


A. Mathayo 23:23 Ole kwa wale wameacha rehema.
B. Hosea 6:6 Mungu anapenda fadhili zaidi ya sadaka.
C. Mathayo 9:11-13 Yesu ataka rehema zaidi ya sadaka.

### XI. Baraka na Hukumu

A. Mathayo 5:7 Heri wenye rehema.
B. Yakobo 2:13 Hukumu isiyo na huruma kwake yeye asiyeona huruma.
C. Mathayo 18:33-35 Mrehemu anayekukosea.

Tamati

*Basi, kwa kuwa mmekuwa wateule wa Mungu, watakatifu wapendwao, jivikeni moyo wa rehema, utu wema, unyenyekevu, upole, uvumilivu, mkichukuliana, na kusameheana, mtu akiwa na sababu ya kumlaumu mwenzake; kama Bwana alivyowasamehe ninyi, vivyo na ninyi. —Wakolosai 3:12-13*



# Mwingi wa Rehema

Watu wengi humtazama Mungu kama kiumbe cha kiungu ambaye ameshika upanga wa hukumu ambao uko tayari kuwakatakata watu kwa makosa madogo ya kiroho. Lakini uelewaji wa aina hii wa Mungu uko mbali sana na ukweli, kwa maana Mungu ni mwenye rehema. Mikono yake ya rehema imenyooshwa ili kuwasaidia watu wote wakati wamejipata dhambini, katika hali ya kuanguka, ya kuwa wahitaji, ya kuteseka, na hata ya majaribu.

## Sifa ya Mungu

Mwanazaburi aliandika na kusema "Lakini Wewe, Bwana, u Mungu wa rehema na neema, mvumilivu, mwingi wa fadhili na kweli" (Zaburi 86:15). Rehema ni mwelekeo wa kuwa mwenye huruma, kuwa tayari kutoa msamaha. Ni sifa inayoambaa na huruma, msamaha, na kutokuwa na ukali na watu, mahali ambapo ni hukumu ingetolewa. Rehema, ikiwa sehemu ya neema, ni kipawa cha upendo na huruma zake Mungu, ambazo kamwe hatustahili; Yeye hawapi watu adhabu wanayostahili.

Mara nyingi rehema za Mungu hazitambuliwi, au zinaonekana kuwa hafifu. Mungu sio tu "Mungu wa faraja zote" bali pia Yeye ni "Baba wa rehema" (2 Wakorintho 1:3). Rehema ni sifa ya kimsingi ya Mungu. "Rehema na msamaha ni kwa Bwana Mungu wetu" (Danieli 9:9). Mungu ni wa haki na ni mtakatifu, lakini pia rehema na msamaha ni wake. Rehema ni sehemu kamili ya sifa zake Mungu, kwa maana Yeye ndiye chimbuko la rehema.

"Mungu ni wa haki na ni mtakatifu, lakini pia rehema na msamaha ni wake. Rehema ni sehemu kamili ya sifa zake Mungu, kwa maana Yeye ndiye chimbuko la rehema."

Mara nyingi Maandiko yanatoa mifano mikubwa ya rehema za Mungu katika mahusiano yake na wanadamu. Wakati watu wako taabani na wanamtafuta Bwana, Yeye hatawaachilia, "Kwa kuwa BWANA, Mungu wako, ni Mungu wa rehema" (Kumbukumbu 4:31). Katika Mika 7:18 nabii huyo aliandika maneno mazuri kabisa, "Ni nani aliye Mungu kama wewe, mwenye kusamehe uovu, na kuliachilia kosa la watu wa urithi wake waliosalia? Hashiki hasira yake milele, kwa maana Yeye hufurahia rehema." Naye Kristo alidhihirisha hali hiyo halisi ya rehema zake wakati alipokuwa akiwahudumia wenye dhambi huku akitembea humu duniani. "Na alipowaona makutano, aliwahurumia" (Mathayo 9:36).

## Rehema Zake Mungu Ni Nyingi na za Kudumu

Mungu "Haoni hasira upesi, ni mwingi wa fadhili" (Zaburi 103:8). Kuna ghala la rehema ambalo ni kuu zaidi kuliko wito wa hukumu. Hapo kwa rehema ndipo Daudi aliitana baada ya kutenda dhambi na Bathsheba. Daudi alikuwa amevunjika, mtu mwenye hatia, na aliyejaa toba. Ndipo akaomba, "Ee Mungu, unirehemu, sawasawa na fadhili zako. Kiasi cha wingi wa rehema zako, uyafute makosa yangu" (Zaburi 51:1). Kiasi cha wingi wa rehema za Mungu kinamaanisha kwamba rehema hizi ziko tayari kutolewa, ni nyingi, na kwamba Yeye ana mwelekeo wa kuwa na huruma nyingi. Wito wa Daudi haukuwa wa kufanyika haki, bali tumaini lake lilikuwa katika rehema zake Mungu ambazo hazina kipimo. Kwa rehema hizi Mungu kwa sasa anachelewesha hukumu ya mwisho ili kutoa nafasi zaidi kwa watu kuokoka. Bwana "Huvumilia kwenu, maana hapendi mtu ye yote apotee, bali wote wafikilie toba" (2 Petro 3:9).

## Wote Wamefanya Dhambi na Wanastahili Hukumu

"Wote wamefanya dhambi" (Warumi 3:23), wamefanya makosa, na kuvunja amri zake Mungu. Kutokana na dhambi hii sisi sote tunastahili hukumu, kwa maana "mshahara wa dhambi ni mauti" (Warumi 6:23). Lakini hata wakati tulikuwa katika hali hiyo ya kutostahili, Mungu alitunyooshea upendo na rehema zake kupitia Yesu Kristo. "Lakini Mungu, kwa kuwa ni mwingi wa rehema, kwa mapenzi yake makuu aliyotupenda; hata wakati ule tulipokuwa wafu kwa sababu ya makosa yetu; alituhuisha pamoja na Kristo; yaani, tumeokolewa kwa neema" (Waefeso 2:4-6). Rehema hazitokani na na mapenzi ya mwanadamu, bali zinatokana na mapenzi makuu ya Mungu (Warumi 9:15-16). Mwanadamu hastahili rehema, pia hawezi kustahili rehema kwa bidii zake mwenyewe. Rehema ni kipawa kutoka kwake Mungu.

## Wokovu na Uzima wa Milele Unapatikana kwa Rehema

Ni kutokana na upendo ndipo Mungu alimtuma Yesu ili kufa kwa ajili ya dhambi za wanadamu. Wokovu ulikuja, "Si kwa sababu ya matendo ya haki tuliyoyatenda sisi; bali kwa rehema yake" (Tito 3:5). Wokovu hauji kwa wale wamehitimu kutokana na wema au utakatifu wao. Badala yake wokovu huja kwa mwenye dhambi

*(Endelea katika Ukurasa 6)*

(Inaendelea kutoka Ukurasa 5)
mkubwa ambaye atatubu na kukubali kipawa hiki cha Mungu.Wakati mtu mwovu anaachana na njia zake na kumrudia Bwana, "Naye atamrehemu; na arejee kwa Mungu wetu, naye atamsamehe kabisa" (Isaya 55:7). Mtu ambaye anajihisi hastahili upendo na msamaha wa Mungu kwa sababu ya makosa ya kale atakubaliwa na kupatanishwa na Mungu kutokana na rehema zake.

## Rehema Ndizo Huwadumisha Watu wa Mungu

Daudi aliandika na kusema: "Niliposema, mguu wangu unateleza; ee BWANA, fadhili zako zilinitegemeza" (Zaburi 94:18). Kwa watu ambao wanajaribu kumtumikia Mungu kutakuwa na nyakati za kuanguka na kufanya makosa. Lakini Mungu kamwe hatamweka mtu mbali naye kwa sababu hakuishi maisha makamilifu; badala yake Yeye atamsaidia mtu huyo na kumpatia nguvu mpya. Mungu ndiye humrudishia mtu hali bora inayofaa na kuwashikilia watu wake kwa rehema zake, ndipo wasiingie kwenye maangamizi. Wakati maisha yameingia giza na mambo yanaonekana kwenda mrama hebu tumkumbuke nabii Yeremia, "Najikumbusha neno hili, kwa hiyo nina matumaini. Ni huruma za BWANA kwamba hatuangamii, kwa kuwa rehema zake hazikomi. Ni mpya kila siku asubuhi; uaminifu wako ni mkuu" (Maombolezo 3:21-23).




> "Wakristo hawastahili 'kuwa' tu na rehema, bali kwamba wanastahili 'kupenda' rehema. Rehema hutilia maanani zaidi ya hisia za mtu binafsi, na kutambua hisia na mahitaji ya watu wale wengine" (1 Yohana 1:9).

## Kuhani Mkuu Mwenye Rehema

Yesu alifanyika kuwa katika hali ya mwanadamu ili, "apate kuwa kuhani mkuu mwenye rehema" (Waebrania 2:17). Yeye anaelewa ugumu wa kuwa katika mwili, na anawarehemu watu wakiwa katika makazano yao. Sisi wanadamu tunaweza kwenda kwake tukiwa na hakikisho lake kama kuhani mkuu, na "tupewe rehema, na kupata neema ya kutusaidia wakati wa mahitaji" (Waebrania 4:16).

## Mwisho wa Rehema za Mungu

Katika maisha haya Mungu ako tayari kabisa kuonyesha rehema, kuliko kuleta hukumu. Lakini ni makosa kwetu kupuuzilia uhalisi wa hukumu inayokuja, wakati ambapo kutakuwa na mwisho wa rehema zake Mungu. Hukumu itakuja kwa wale ambao wamemkataa Yesu na maneno yake (Yohana 12:48). Kutakuwa na adhabu ya milele (Mathayo 25:45-46) kwa wale ambao wamekataa kukubali rehema na wokovu wake Mungu. Kama vile ambavyo wale waliodharau sheria ya Musa waliuawa bila rehema, ndivyo itakavyokuwa kwa wale ambao wamedharau damu ya wokovu wake Yesu (Waebrania 10:28-29).

Hebu basi tumshukuru Mungu kwa rehema zake! Kupitia kwa upendo na msamaha wake, wakati ambapo tumetubu, badala ya kupata adhabu ambayo tunastahili, tutaweza kupata tumaini, amani, na kurudishiwa hali bora ya mahusiano. Mungu hampendelei mtu yeyote, na rehema zake zimetolewa kwa watu wote, bila kujali walikotoka, au hata shida walizo nazo.

## Tumeitwa Ili Tuishi Maisha ya Rehema

Vile ambavyo Mungu ni wa rehema sisi wafuasi wake tunastahili kuwa watu wa rehema. Yesu alitoa mwongozo dhabiti ambao tunastahili kufuata, "Basi, iweni na huruma, kama Baba yenu alivyo na huruma" (Luka 6:36). Mika 6:8 inatuuliza swali, "BWANA anataka nini kwako, ila kutenda haki, na kupenda rehema . . ." Wakristo hawastahili "kuwa" tu na rehema, bali kwamba wanastahili "kupenda" rehema. Rehema hutilia maanani zaidi ya hisia za mtu binafsi, na kutambua hisia na mahitaji ya watu wale wengine. Katika hali kamilifu ya rehema mtu hatoi rehema shingo upande, au kama wajibu wa lazima tu, bali kwa wingi wake na kutoka moyoni mwake.

## Rehema Ni Bora Kuliko Sadaka

Ilhali kuna wakati wa kutolewa kwa hukumu ya haki, mtoto wa Mungu anahitaji kutilia mkazo zaidi swala la kuwarehemu watu wale wengine, ambao hawaishi maisha yanayopendeza. Kama walivyokuwa wakifanya Mafarisayo, Wakristo wengi wanatilia maanani utakatifu unaoonekana kwa nje, na kupuuza maswala yaliyo makubwa ya rehema (Mathayo 23:23). Agano la Kale (Hosea 6:6) na pia Agano Jipya (Mathayo 9:11-13) zinadhibitisha kwamba Mungu anapendelea rehema kuliko sadaka. Roho wa rehema ni muhimu ZAIDI kushinda sadaka za kuonekana zinazotokana na maisha matakatifu. Hukumu huwatupa watu mbali, ilhali rehema huvutia watu na kutoa mweke kwao ili waweze kubadilika.

Wakati watu wamefanya makosa au hata kutenda dhambi, sisi wateule tunahitaji kuwasiliana nao na kuwashughulikia kutokana na msimamo wa rehema na msamaha. Sisi sote tulihitaji na tungali tunahitaji rehema zake Mungu. Je, inawezekanaje sisi watoto wa Mungu kuwa na rehema za kiwango kidogo zaidi kwa wenye dhambi na kwa Wakristo wale wengine?

## Baraka na Hukumu

Yesu alisema, "Heri wenye rehema; maana hao watapata rehema" (Mathayo 5:7). Ikiwa mtoto wa Mungu hataishi maisha ya kuwaonyesha wenzake rehema, Mungu naye atamhukumu bila rehema (Yakobo 2:13). Ikiwa wafuasi wa Yesu hawatawasamehe wenzao wanapowafanyia makosa, na kuwarudishia uhusiano bora, Mungu naye hatawasamehe makosa yao (Mathayo 18:33-35).

Maishani mwetu tunahitaji sana rehema zake Mungu, ndiposa sisi nasi tunahitaji kuwa tayari kabisa kuwarehemu watu wale wengine walio karibu nasi. ■

# Maswali na Majibu

## Je, nawezaje kuwa na rehema halisi wakati mtu ananitumia vibaya?

Mtu kuwa na roho ya rehema sio kumaanisha kwamba uwaruhusu watu kukutumia vibaya. Ikiwa mtu atanipiga konde shavuni, mimi nahitaji kumgeuzia shavu lingine, kama ambavyo Yesu alitufundisha. Kamwe sistahili kulipiza kisasi, bali nahitaji kustahimili kufanyiwa makosa kama hayo; lakini kwa kweli mimi nitamwondokea mtu kama huyo, ikiwezekana kufanya hivyo. Wakati umati ulitaka kumbingirisha Yesu kutoka kilimani, Yeye aliponyoka katikati mwao.

Kama mtu ananitumia vibaya, aidha kimwili, kifedha, au vinginevyo, ni muhimu kutambua usawa wa mafundisho ya Biblia. Sehemu moja ya kutoa rehema ni kumsamehe mtu yule ambaye ametudhulumu. Tunahitaji kumkabidhi mikononi mwake Bwana, na kumsamehe kabisa, haijalishi ni mara ngapi watatufanyia makosa hayo. Lakini hii si kumaanisha kwamba tunahitaji kumkaribisha muuaji huyo nyumbani mwetu, ambapo watoto wetu waliko, na pia hatustahili kumpatia mwizi funguo za nyumba yetu. Sisi tunahitaji kuwa wasimamizi bora wa kile ambacho Mungu ameweka mikononi mwetu. Jambo hili wakati mwingine litamaanisha kwamba tunahitaji kuweka viwango vya kupima mambo yote, na pia kuwa na miongozo na kuweka mipaka ambayo haina budi kudumishwa. Katika nyakati kama hizo, daima tunahitaji kudumisha roho wa upendo. Katika mahali ambapo hapafanyiki haki ulimwenguni, tunahitaji kutambua kwamba rehema zetu hazina nguvu za kuleta mapatanisho, bali kwamba rehema hizo hutoa tu mweke kwa mapatanisho kufanyika.

## Je, unawezaje kudumisha kiwango cha ukweli huku ukiwaonyesha wanadamu wenzako rehema?


Nafsi yangu imo mikononi mwangu. Mimi sina nguvu za kuwabadilisha watu wale wengine, lakini nina nguvu kutokana na neema za kuweza kuishi maisha matakatifu mbele zake Mungu, kwa kulingana na ukweli. Hatustahili kulowesha maji utakatifu wa maisha yetu kwa ajili ya kuwapendeza watu wale wengine ambao wametuzunguka. Lakini sehemu moja ya kiwango hicho cha ukweli ni sisi kuwaonyesha rehema wenzetu hao ambao hawaishi maisha matakatifu. Tunahitaji kufanya bidii kuonyesha upendo watu wale wengine ambao hawaishi maisha ya utauwa.

Somo muhimu ambalo Wakristo wanahitaji kujifunza ni kwamba, kuwakubali watu sio kumaanisha kwamba unakubaliana na matendo yao. Tunaweza kumkubali mtu na kumpenda bila kukubali matendo yake. Hebu zingatia kwamba, ikiwa hakuna ukweli ambao tunastahili kuudumisha basi hakutakuwa na haja ya kunyoosha mkono wa rehema kwa watu wale wengine. Rehema hazihitajiki kwa mtu ambaye anafanya mambo sawasawa; zinahitajika kwa yule ambaye anafanya makosa.

Zaburi 85:10 inasema kwamba, "Fadhili na kweli zimekutana, haki na amani zimehusiana." Ukweli wa utakatifu humulika dhambi na kudai hukumu. Lakini kwa upande mwingine, rehema hutafuta amani na kurudishia watu uhusiano bora. Kupitia kwa Kristo kweli na rehema zilipatana hapo Kalvari, na mahali hapo ndipo tulipata wokovu. Nasi pia tunatakiwa kwamba rehema na kweli zipatane maishani mwetu. Hebu basi tuhubiri, tujifunze, na tuishi maisha kulingana na ukweli, ili wenzako waone njia ya kweli; lakini pia hebu uwaonyeshe rehema na huruma, hata katika kupotea huko kwao. Rehema ndizo zinazowavutia watu kwa ukweli, na si roho ya utakatifu wa kibinafsi.

Kweli na rehema, hukumu na rehema, haya si mambo ambayo haingiliani. Kama Kristo alivyofundisha, kufanya hukumu za haki si kwenda kinyume na rehema.

---



Njia zote za BWANA ni fadhili (rehema) na kweli, kwao walishikao agano lake na shuhuda zake. —Zaburi 25:10

Kama ambavyo barabara huwa na alama za kubondeka katika mahali ambapo gari la kuvutwa na farasi linakopitia, ndivyo ambavyo alama za njia ya kupitia ambayo humfikisha mtu kwa Kristo zinavyotakiwa kuwa. Wakristo wanalo jukumu, sio tu la kutambua njia ya kweli, bali pia njia ya rehema.

JE, WAJUA?

*Hizi ni ishara kwamba wewe unahawakumu watu wale wengine:*

1. Unapokutana na watu, unawakagua kwa makini ili kuwatoa makosa.

2. Una “hasira kubwa zaidi” kwa makosa na dhambi za watu wale wengine, kuliko jinsi unavyoona aibu kwa makosa yako mwenyewe.

3. Huwaweki watu wale wengine huru (kwa haraka) kutokana na makosa yao.

4. Unakosa kutilia maanani au kujitenga kutoka kwa watu ambao hawakubaliani nawe, au hamfanani kimawazo.

5. Uko tayari kusema maoni yako kuhusu mahitaji ya watu wale wengine, au kuhusu upungufu wao wa kukosa kuwa watu wa kiroho.

6. Unashindwa kuona mbali zaidi ya makosa ya watu wale wengine.

Neno Linalofaa kwa Msimu Huu

# UJUMBE KUTOKA KWA KITI CHA REHEMA

*Nami nitaonana nawe hapo, na kuzungumza nawe pale nilipo juu ya kiti cha rehema.* —Kutoka 25:22



Wakati wana wa Israeli walipokuwa wakitembea jangwani, walikuwa wakibeba Hema, ambayo ilikuwa ni kijisanduka cha kubebwa. Sanduku la Agano liliwekwa Mahali Patakatifu Sana, ambapo ndipo palikuwa sehemu ya ndani sana ya hema. Juu ya sanduku hilo kulikuwa na kifuniko ambacho kilikuwa chajulikana kama kiti cha rehema. Hapo ndipo Mungu alinena na Kuhani Mkuu, mara moja kwa mwaka, kwenye Siku ya Upatanisho. Ni baraka na faraja kuu kiasi gani kujua kwamba Mungu aliwashughulikia watu wake kutoka kwa kiti cha rehema, badala ya kiti cha hukumu. Bila kuzingatia dhambi ilikuwa ya aina gani, mradi tu damu imetumika, Mungu alinyoosha rehema zake na msamaha wake kwa wana wa Israeli.

Hata ingawa damu ya fahari na mbuzi haikutosha kuondoa dhambi, Yesu alikufa msalabani kulipia dhambi ya wanadamu wote. Katika kipindi hiki cha Agano Jipya tungali twaweza kukaribia kiti cha enzi cha Mungu, ambapo atanena nasi kutoka kwa kiti cha rehema na upendo. Hata ingawa kutakuwa na dhambi au makosa, kila mmoja wetu tunaweza kuja kwa Kristo. ambaye atakuwa daraja la kivukio hadi kufika kwake Mungu kupitia kwa rehema zake. Badala ya kutoa hukumu na maangamizi, Yeye atatuletea njia ya uponyaji na kupata patanisho. Kamwe hatustahili kuogopa kukaribia kiti cha rehema cha Mungu, maana hapo ndipo tunaweza kuwasiliana na Mfalme wa Wafalme.

Tumebarikiwa sana kupata mweke na hakikisho la kuwasiliana na Mungu kutoka kwa kiti chake cha rehema. Sisi nasi kama watoto wa Mungu huwa na mahusiano mengi na watu ambao wametuzunguka – familia, marafiki, wakristo wenzetu, wafanyi kazi wenzetu, n.k. Je, sisi huhusiana nao kutoka kwa kiti gani? Je, tunahusiana nao na kufanya maamuzi maishani mwetu kuwahusu kutoka kwa kiti cha hukumu, au kutoka kwa kiti cha rehema?

Tunahitaji kufuata nyayo za Yesu na kushiriki asili yake ya kiungu. Kama Mungu huwasiliana nasi kutoka kwa kiti cha rehema, je, twawezaje kuwa wakali na wenye mwelekeo wa hukumu kwa matendo yetu na hata rohoni mwetu kwa watu wale wengine? Hebu basi tuwasiliane na watu wote kutokana na mwelekeo wa rehema ili wapate kumwona Yesu ndani yetu, na wapate njia ya uponyaji na patanisho. ■

Anwani

The Gospel Truth
P. O. Box 2042
Nixa, MO 65714
USA

Email:
editor@thegospeltruth.org

Utakatifu kwa Bwana